TANGAZO LA SERIKALI NA. 321 la tarehe 25/08/2017

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya Kifungu vya 7(1) na 16 (1)

_____

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA, MWAKA 2017

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha magari ya abiria na mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga;

"Karakana" maana yake ni eneo la Halmashauri lililotengwa kwa ajili ya shughuli za ufundi na kuhifadhi vyombo vya usafiri;

"Kituo cha basi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kutolea huduma za usafiri ambapo mabasi au vyombo

vingine vya usafirishaji wa abiria vitapakia au kushusha abiria na mizigo yao;

"Maegesho" maana yake ni sehemu iliyotengwa maalum ya kuegesha magari;

"Mitaa" maana yake ni barabara, njia au eneo la umma ambapo Halmashauri inaweza kuainisha kuwa sehemu ya maegesho;

"*Maegesho ya hifadhi"* maana yake ni maegesho yaliyohifadhiwa kwa watu maalum.

Ushuru wa maegesho

4. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi na maegesho ya vyombo vya usafiri vitakavyoegeshwa katika maeneo maalum yatayotangazwa kuwa ni maeneo ya maegesho kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Jedwali la kwanza.

(2) Ushuru wa maegesho ya magari utatozwa kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni kila siku isipokuwa siku ya Jumapili.

(3) Ushuru wa maegesho ya magari unaweza kulipwa kwa kila saa, siku au mwezi kulingana na makubaliano kati ya Halmashauri au wakala wake na Mlipa ushuru.

(4) Endapo mtu atakuwa amelipia ushuru wa maegesho kwa siku au kwa mwezi ataruhusiwa kuegesha chombo chake cha usafiri katika eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya maegesho kwa muda aliolipia bila kudaiwa tena.

Sehemu za maegesho

5. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mitaa yote ya katikati ya mji (Central Business District) itakuwa ni sehemu za maegesho ya vyombo vya usafiri.

(2) Halmashauri inaweza kugawa maeneo ya maegesho kwa mistari au kwa kutumia alama yoyote itakayoonyesha idadi na sehemu ambayo chombo cha usafiri kinatakiwa kuegeshwa.

(3) Halmashauri au wakala wake anaweza kuainisha baadhi ya maeneo katika Mitaa kuwa ni sehemu ya maegesho yaliyohifadhiwa.

Kituo cha mabasi

6. (1) Itakuwa ni marufuku kwa basi la abiria kushusha ama kupakia abiria nje ya vituo vya mabasi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa kituo cha mabasi kutoka kwa kila mmiliki wa basi ambao utalipwa wakati basi linapotoka kituoni kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Safari zote za mabasi zitaanzia kwenye vituo vya mabasi isipokua kwa mabasi yanayopita kutoka maeneo mengine ya nje ya Halmashauri.

(4) kwa lengo la kushusha au kupakia abiria na mizigo yao, mabasi hayataruhusiwa kusimama kwa zaidi ya dakika tano katika vituo vya njiani baada ya kuanza safari zake katika Kituo cha Kikuu cha Mabasi.

(5) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya matengenezo au kuosha gari katika Kituo cha Basi.

Ushuru wa kulaza gari kituoni

7. Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza gari kwenye kituo cha mabasi kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Maegesho yaliyotengwa

8. (1) Halmashauri au Wakala wake anaweza kutenga eneo la maegesho kuwa ni *"maegesho yaliyohifadhiwa"* baada ya kupokea maombi toka kwa Mtu anayetaka kutengewa eneo la kuegesha gari.

(2) Baada ya maombi yake kukubaliwa na kulipia ushuru wa maegesho, ataruhusiwa kutumia sehemu hiyo yeye peke yake bila ya kuingiliwa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) hapo juu mtu yeyote ambaye amelipa ushuru wa maegesho yaliyotengwa atatozwa ushuru wa maegesho endapo ataegesha gari nje ya sehemu aliyotengewa.

(4) Halmashauri inaweza kuzuia magari kuegeshwa katika baadhi ya maeneo kwa kuweka alama au kibao kilichoandikwa.

"HAIRUHUSIWI KUEGESHA HAPA" au "NO PARKING" kwa sababu zifuatazo:-

(a) kwa ajili ya kurahisisha mzunguko wa magari au kwa sababu za kiusalama;

(b) katika eneo hilo kuna ujenzi au ubomoaji unaofanyika;

(c) au kwa sababu nyingine yeyote ile ambayo kama magari yataegeshwa itakwamisha shughuli ambazo zinafanyika katika eneo hilo.

Kushindwa kulipa ushuru

9. (1) Mtu yeyote ambaye:-

(a) atakataa au kushindwa kulipa ushuru; au

(b) ataegesha gari kwa muda mrefu zaidi ya ule aliolipia ushuru atakuwa anatenda kosa.

(2) Endapo mtu yeyote atatenda makosa yaliyoainishwa katika kifungu cha (1) hapo juu Halmashauri au Wakala wake atalifunga gari hilo kwa minyororo hadi hapo mtu huyo atakapolipia ushuru anaodaiwa.

(3) Gari ambalo litakuwa limefungwa mnyororo zaidi ya saa mbili bila ya kulipiwa, litavutwa na kupelekwa

kwenye karakana (Yard) ya Halmashauri kwa gharama za mwenye gari, na Halmashauri haitahusika kwa namna yoyote ile na uharibifu utakaotokea wakati wa uvutwaji huo.

(4) Gari ambalo litakalovutwa na kuhifadhiwa kwenye karakana litakombolewa baada ya Mwenye gari;-

(a) kulipa ushuru anaodaiwa, gharama za uvutaji, pamoja na gharama nyingine ambazo kwa namna moja au nyingine Halmashauri au wakala wake watakuwa wameingia;

(b) kutoa uthibitisho wa umiliki wa gari hilo.

(5) Gharama za uvutaji wa gari itakuwa ni shilingi 30,000/= kwa gari na gharama za utunzaji itakuwa ni shilingi 10,000/= kwa siku.

Gari lililotelekezwa

10. (1) Gari ambayo litakalokaa karakana (Yard) kwa muda wa siku kumi na nne bila kukombolewa, litahesabika kama gari ambalo limetelekezwa.

(2) Baada ya siku kumi na nne kupita Halmashauri itapeleka maombi Mahakamani ili iweze kutamka kuwa gari hilo limetelekezwa na kutoa kibali gari hilo liuzwe kwa mnada wa hadhara.

(3) Fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya gari hilo zitatumika kulipia ushuru anaodaiwa, gharama za kulitunza gari hilo pamoja na gharama nyingine ambazo Halmashauri au wakala ameingia.

Msamaha

11. Halmashauri inaweza kutoa msamaha wa kulipa ushuru wa maegesho kwa chombo cha usafiri ambacho:-

(a) kinamilikiwa na Serikali, Wanadiplomasia, au Jeshi;

(b) gari ya wagonjwa (*ambulance*), gari ya zimamoto,

(c) gari ambalo linamshusha au linamchukua mtu ili

mradi lisikae zaidi ya dakika tano; au

(d) limeegeshwa katika sehemu za kuabudia wakati wa Ibada.

Makosa

12. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

(a) ataegesha gari bila kulipia ushuru wa maegesho;
(b) ataegesha gari nje ya mstari uliochorwa kuainisha eneo la kuegeshea gari;
(c) ataosha gari au kufanya matengenezo katika sehemu za kuegesha gari;
(d) ataegesha gari katika eneo ambalo halijaruhusiwa kuegesha gari; au
(e) atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

13. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya kiasi kisichopungua laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (Tsh.500, 000/=) Mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

_____

JEDWALI LA KWANZA

_____

USHURU WA STENDI

(Yameundwa chini ya Kifungu cha 4(1)

Na.	*Chombo cha usafiri*	*Ushuru wa maegesho*
1.	Teksi	500/= kila inapotoka
2.	Noah	1000/= kila inapotoka
2.	Lori chini ya tani 7/ Pick up/ Basi dogo	3,000/= kwa siku
3.	Lori zaidi ya Tani 7/ Basi kubwa	5,000/= kwa siku
4.	Magari mengine yasiyo ya biashara	500/=kwa siku
5.	Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi 1. Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25 2. Mabasi yanayobeba abiria chini ya 25 mpaka 15	 2,000/= kwa siku 1,500/= kwa siku

_____

JEDWALI LA PILI

_____

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya kifungu cha 16)

Mimi…… wa S.L.P. ……. nakiri kutenda kosa la …….. ikiwa ni kinyume na kifungu cha …… cha Sheria ya Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha magari ya abiria na mizigo) za Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga za Mwaka 2017.

Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwaa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ……...

Mbele yangu:-

Jina: ……..…..

Saini: ……..…..

Wadhifa: ……...

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya ULANGA, umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga uliofanyika tarehe 29. 01.2016 na Mhuri huo ulibandikwa mbele ya:-

YUSUF D. SEMUGURUKA,
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga

FURAHA F. LILONGELI,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga

NAKUBALI

Dodoma,
13 Julai, 2017

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.),
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI